Kusalimia Kwa Busu Takatifu (Greeting With A Holy Kiss)

Na

Alex S. Sadat

Kusalimia Kwa Busu Takatifu

Na

Alex S. Sadat

Aprili 21, 2017

Kusalimia Kwa Busu Takatifu

Rum. 16:3-16

Kwenye mistari 3-16, mtume Paulo anadhihirisha salamu yake binafsi kwa Wakristo katika mji wa Rumi. Sasa, kwenye msitari wa 16 anafanya vitu viwili; sehemu ya mwisho wa msitari huu anaonyesha salamu kutoka kwa Wakristo wote wa Kanisa la Kristo, wale wanao abudu kimaandiko na binafsi naamini kwamba Paulo anafanya hili kwa sababu ya umoja au umuhimu wa umoja ulikuwepo miongoni mwa makanisa ya Kristo kama Bwana wetu analivyoelekeza na kwa sababu ya umoja wetu na Bwana. "*Nanyi mlikuwa wafu kwa sababu ya makosa ya dhambi zenu; ambazo mlizitenda zamani kwa kuifuata kawaida ya ulimwengu huu, na kwa kumfuata mfalme wa uwezo wa anga, roho yule atendaye kazi sasa katika wana wa kuasi; ambao zamani sisi nasi tulienenda kati yao katika tamaa za miili yetu, tulipoyatimiza mapenzi ya mwili nay a nia, tukawa kwa tabia yetu watoto wa hasira kama na hao wengine…*" (Efe. 2:1-22). Anaonyesha salamu kwa niaba ya makanisa haya kwa sababu alikuwa na ukaribu na wengi wao na pia mahusiano yasiyo ya moja kwa moja. "*Baghairi ya mambo ya nje yako yanijiaayo kila siku, ndiyo maangalizi ya makanisa yote.*" (2 Kor. 11:28). Ni kama Ellis alipokuja Afrika Mashariki na kuieneza Injili ya Yesu Kristo kulingana na agizo kuu, anayafahamu makanisa aliyoyaacha hapa Afrika na baadhi ya majina ya waumini katika makanisa hayo. Kwa nyongeza, kujihusisha kwa Paulo, kwa makanisa yote kama mtu yeyote anavyoweza kujihusisha leo na makanisa alikuwa anaweza kichukua changizo kwa ajili ya watakatifu maskini kule Yerusalemu, na kila kanisa lililochangia anaonekana kutuma muwakilishi binafsi pamoja na Paulo, (1 Kor.16:2-4).

Jambo la kwanza tunaloliona kwenye msitari wa 16 ni agizo, la **kusalimiana kwa busu takatifu** ninaamini kwamba hii ni salamu binafsi. Makanisa yote yanatuma salamu zao (ms.16b). watenda kazi wenza wa Paulo pia walituma salamu zao (ms 21-23). Na sasa anawaambia Wakristo wa rumi kusalimiana wao kwa wao

(ms16a), tunapaswa kuweka akilini kwamba salamu ya Kikristo huonyesha umoja wa Wakristo. Hivyo basi, salamu inapaswa kuwa ndani ya kanisa, vilevile miongoni mwa makanisa. Mtume Paulo analiambia kanisa la Rumi na kila mahali sio tu kusalimiana, lakini anatuambia jinsi gani salamu hii inapaswa kuwa; **kwa busu takatifu.** Kwa wale wanaosoma na kutafakari maandiko wanaweza kuona kwamba agizo hili halipatikani mara moja tu katika Biblia; bali inapatikana mara tano katika Agano Jipya. "*Ndugu wote wawasali salimianeni kwa busu takatifu.*" (1 Kor. 16:20; 2 Kor.13:12; 1 Thes. 5:26 na 1 Pet. 5:14).

- Kila Mkristo lazima na anapaswa kuwa tayari kutii maandiko, sawasawa kama agizo lilivyotolewa na ndio maana tunaitwa Wakristo.
- Katika matukio yoyote zaidi tunavyopenda kukubali, hiki ndicho tunatakiwa kufanya bila udhuru au kuundaunda. Hataivyo, utii rahisi wa maagizo ya Mungu kunapaswa kuwe ndo hamu yetu majibu ya kila wakati.
- Ndugu tunapaswa kukumbuka kwamba kukiwa na agizo kuna hatari ya uhalisia pamoja na kuruhusu kila jambo vitu ambavyo tunapaswa kuviepuka kwa sababu ni hatari. Kumtii Mungu ni zaidi ya kutunza sheria, kutii sheria ya Mungu na sheria ya binadamu lakini utii huo kunafaa kuwepo motisha. Tunapotunza sheria hatuwi kwa mwonekano wan je bali wa ndani pia. Ndugu utii unapaswa kutoka katika moyo mweupe na dhamira njema na tukifanya hivyo baraka zake huja juu yetu.

Hotuba mlimani ilikuwa ni shambulio la Bwana kuhusu sheria kali au kutengeneza sheria na kutunza maagizo ya Waandishi na Mafarisayo. Na alifikiria hotuba yake, akasisitiza kwamba mwanadamu anatakiwa afikirie zaidi ya sheria katika fikira zao na wanapaswa kuendelea mbele katika yale wanayotakiwa kufanya. Mtume Paulo alielewa hii vizuri sana nasi tunapaswa kufanya vivyo bhivyo. Moja ya vitu alivyoelewa ilikuwa ni agizo usimfunge ng'ombe apurapo nafaka ilikuwa juu ya kanuni ya marekebisho. "*Kwa maana katika torati ya Musa imeandikwa, usimfunge kinywa ng'ombe apurapo nafaka. Je! Hapo Mungu aangalia mambo ya ng'ombe? Au yamkini anena hayo kwa ajili yetu? Naam yaliandikwa kwa ajili yetu; kwa maana alimaye nafaka ni haki yake kulima kwa matumaini, naye apuraye nafaka ni haki*

yake kutumaini kupata sehemu yake." (1 Kor. 9:9-10). Kama mtu atatii sheria kwa njia ambayo itampendeza Mungu, basi hii inatakiwa kwendana na kanuni zilizopo chini yake. Pia itamanisha kwamba utii wa kanuni mara zote itahitaji kinachofanana na kutojali kanuni. Kwa mfano, Yesu alidhihakiwa kwa kuvunja Sabato, lakini alijihami kwa kuwakumbusha wale waliokuwa wanamdhihaki kuhusu kanuni muhimu; kwamba sabato ilifanywa kwa ajili ya mwanadamu, na siyo mwanadamu kwa ajili ya Sabato (Mat. 12:8-9). Hataivyo, tunapaswa kukumbuka kwamba Sabato ilianzishwa kwa ajili ya faida ya mwanadamu na hivyo, Yesu kuponya au kufanya lolote siku ya Sabato ilikuwa sahihi, hataivyo ilikuwwa ni kazi. (Mat.12:1-8). Mtu mmoja katika Agano la Kale, Daudi alikula mkate mikate ya wonyesho na akawapa watu wake, kitu amabcho hakikuwa sheria kufanya kulingana na maandiko na sheria ya Musa inakataa. Tena kanuni ya juu ilifanya hili kuwa kutotii kwa wazi. (Mat. 12:1-2). Uhalishwaji unaweza tu kuona kanuni, lakini Bwana aliwafundisha mitume wake kama jinsi anavyotufundisha leo katika neno lake kuangalia sababu na kulitii kwa sababu ya

- Ninaamini kuna sababu ambazo zinaweza kutuhitaji kutii agizo la Paulo ambayo pia ni maagizo ya Bwana kwa njia tofauti kuliko kwenda unabusu kila mtu. Tunafanya anachotuambia Paulo kwa sababu alipokea kwa Bwana. Na kanuni ya juu ni kwamba Biblia inazungumzia ni kukataa kila aina ya ubaya. (1 Thes. 5:22). Katika desturi zetu za Kiafrika, kubusu kunaweza kumanisha kitu kingine tofauti na kile ilichokuwa ikimanisha katika kanisa ya karne ya kwanza. Kama kumbusu mtu kunaweza kumfanya ajikwae au kufanya hatia kwa injili, basi haipaswi kuwa kitu sahihi kufanya.
- Agizo fulani au tendo inayoonekana kuvunja kanuni iliyopatikana, hivyo tunapaswa kutafuta njia sahihi inayowezekana na kuitimiza kwa njia sahihi kanuni hiyo.
- Ukweli mzuri unaoegemea kifungu chetu na agizo la Bwana ni ule wa umoja wa Kristo. Agizo la kusalimiana kwa busu takatifu limetolewa ili kuhakikisha umoja unaonyeshwa katika kanisa. Kinyume cha hii ni kukataa kuwapokea wengine, hasa wale wanao tofautiana nasi katika mambo ya ushawishi. (Rum. 14:1; 15:7). Nyakati za Paulo na katika

mila, “kusalimiana kwa busu takatifu” kuliwafanya Wakristo kufanya kile ambacho hakikuwa cha asili na hata kidesturi haikukubalika. Tena, tunapaswa kukumbuka kwamba “busu takatifu” ni ishara ya umoja na mshikamano.

Desturi zetu za kiafrika hasa watu wanaposhindana kwenye chaguzi, wale wote wanaogombea hawasalimiani kwa mkono kwa sababu kuna chuki na uhasama. Lakini salamu inayozungumziwa katika Warumi 16:16 ni kwa ajili ya umoja na upendo wa Agape.

Paulo alifanya kazi kubwa kuonyesha umoja uliopo mingoni mwa Wakristo. Bila kujali rangi, au hali yao kiuchumi. Agizo la kusalimiana kwa busu takatifu ni himizo la kuonyesha umoja huu katika njia ya msshikamano na kwa njia ambayo sio ya chuki na inayoleta ladha. Tunafahamu kwamba watakatifu ambao Paulo aliwasalimia Rumi walikuwa wake kwa waume, Wayahudi na Wayunani, na labda watumwa na huru. Kwa watu waliokuwa tofauti na naamini kwamba wapo ndani ya kanisa la Bwana leo wameshikilia chuki dhidi ya wenzao. Agizo hili lilikuwa ladha halisi la utii. Hivyo nafahamu kwamba kuna nchi ambazo wananchi wake husalimiana kwa busu au Mkristo wa Kiarabu kumbusu Mkristo wa Kiyahudi kwa busu takatifu na Paulo haimizi chochote isipokuwa hiki. Hapa Tanzania, mwanamke anapomsalimia mwanamume au mwenza wake, hupiga magoti. Na sehemu zingine wanaume wanaposalimiana hupiga magoti.

Katika mila zetu, umoja wa Wakristo unaweza usionyeshwe kwa kubusu au kunaweza kusiwe na njia ya sisi kusalimiana kwa busu ambayo hakika ni takatifu. Kama sivyo, tunatakiwa kutafuta njia ambayo tunaweza kuonyesha umoja wetu. Naamini kwamba njia moja wapo ya kuifanya hii ni kufungua milango yetu kwa wale waumini ambao mara zote hawakaribishwi katika sehemu zetu za siri zinazozuiliwa na kuwa na ushirika. Kimila, hii itawashangaza wale wanaotutazama kinyume. Kwa Wakristo, itakuwa njia nzuri kuonyesha umoja mkuu tulionao katika Kristo miongoni mwa tofauti zetu. wengine walioko nje ya imani wanaoweza kudai kwamba nasi ni miongoni mwa mila zao au makundi, nina mashaka kwamba watachukia. Tunakaa katika mafundisho yake tunapofuata yale anayofundisha na kuyafanya. Hivyo basi, umoja wa Wakristo haipaswi kuwa kitu tunachokitangaza tu bali pia tunaionyesha katika mienendo yetu.

Hitimisho

Salaam, ndiyo maandhari ya kifungu chetu na Wakristo wote wanapaswa kusalimiana kwa njia moja au nyingine, ndugu zetu na dada zetu wanapaswa kuonyeshwa kwamba tunawakubali na kuwapokea katika ushirika wetu kwa sababu sisi ni mamoja katika Kristo. Salamu zetu ni za umoja, lakini kuna mantiki nyingi.

Hii inaweza kufanywa kwa wageni katika kusanyiko letu na sio kitu ambacho ni kinyume na maadili au ishara nzuri tunayofanya. Laakini ni tendo muhimu ambayo sisi tulio ndani ya Kristo na umoja wetu na wote walioko ndani ya Kristo. Ndugu hii inanikumbusha Ellis alipokuja Afrika kwa mara ya kwanza, alikuwa akisalimiana kwa mkono kila mtu kaanisani ikiwa kama ishara ya salamu, bila kujali kauli za watu wengine weupe wanaodai kwamba Waafrika ni wachafu, lakini hakuwa na hila kama hizo. Ukiachana na Wakristo wenza, isipokuwa tu katika nidhaamu ya kanisa, ni dhambi kutotiii. Tukishindwa kuwakaribisha kwa ukarimu, tunajikutakatika hali ambayo ni ya ubaguzi ambayo pia hufanana na aina hiyo ya dhambi, lazima tumanishe tunapofanya mambo. Hatupaswi kuwaachia wengine, lakini ni wajibu wetu sote. Katika hili ninaamini kwamba Paulo alitoa muda wake mwingi na juhudi kwa hii salamu za mwisho huko Rumi kulingana na mafundisho yake na matendo yake katika nyaraka zingine kwa makanisa mengine. Watu wanapaswa kuwa nafasi zetu; tunapaswa kupenda na kumtumikia Mungu kuliko kitu kingine chochote na mtu ye yote. Lakini inatakiwa ijifanyie yenyewe katika kuhudumu na kuwapenda wengine, kuweka maslahi yao mbele kuliko yetu tukiwapendeza na siyo sisi wenyewe na kwa kufanya hivyo tunampendeza Mungu.

Watu waliomfahamu Mungu na kumtumikia kwa uaminifu ni furaha ya Wakristo na zawadi yao. Walikuwa kwa ajili ya Paulo kama alivyowaambia; akiwathamini na uhusiano wao kwake. Alitamani sana kuwa nao ili washiriki taabu pamoja naye. Nakumbuka Ellis alipokuwa anarudi kwao, alikuwa na huzuni kwamba alikuwa anatuacha. "*Basi ndugu zangu wapendwa wangu ninaowaonea shauku, furaha yangu na taji yangu, hivyo simameni imara katika Bwana, wapenzi wangu. Namsihi Euodia, namsihi na Sintike, wawe na nia moja katika Bwana.*" (Fil. 4:1-2).

"*Hata mkawa kielelezo kwa watu wote waaminio katika Makedonia, na katika Akaya. Maana kutoka kwenu neno la Mungu limevuma, si katika Makedonia na Akaya tu, ila na kila mahali imani yenu mlionayo kwa Mungu imeenea hata hatuna haja sisi kunena lolote…*" (1 Thes. 1:7-10).

Ni matumaini na maombi yangu kwamba kanisa alilolifia Bwana na ambalo mimi na ndugu wengine hushiriki ifahamike kwa ajili ya upendo wetu kwa Mungu na kwamba tuwe makini na neno la Mungu katika yote tunayoamini na kutenda. Kwa nyongeza ya hii, ninaamini kwamba sisi ni kanisa lililotiwa mhuri wa upendo wetu kwa kila mmoja wetu tunapoonyesha kwamba sisi ni wanafunzi wa Bwana wetu.

Bwana wetu mwema na atusaidie katika yote tunayofanya kwa ajili ya Ufalme wake.